



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
CHAMA CHA MAWAKILI WA SERIKALI TANZANIA



TANGAZO LA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA CHAMA CHA
MAWAKILI WA SERIKALI (PBA)

Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali (PBA) unatarajia kufanyika tarehe 25-26 Juni, 2026 kwa mujibu wa Tangazo lililotolewa na Uongozi wa Chama. Kwa mujibu wa Kanuni za Usimamizi na Uendeshaji wa Chama cha Mawakili wa Serikali T.S. Na. 529 la Mwaka 2019 Uchaguzi wa Viongozi wa Chama cha Mawakili wa Serikali unapaswa kufanyika wakati wa Mkutano Mkuu wa Chama. Katika kufanikisha Uchaguzi huo, imeundwa Kamati ya Uchaguzi ili kuratibu na kusimamia Uchaguzi wa Viongozi wa Chama. Hivyo, Kamati ya Uchaguzi inawatangazia Wanachama wote wa Chama cha Mawakili wa Serikali kuwa kutakuwa na Uchaguzi wa Viongozi wa Chama kwa nafasi zifuatazo-

1. Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali;
2. Makamu wa Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali;
3. Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya Chama cha Mawakili wa Serikali;
4. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya Chama cha Mawakili wa Serikali;
5. Katibu wa Kamati ya Uongozi ya Chama cha Mawakili wa Serikali;
6. Mweka Hazina wa Chama cha Mawakili wa Serikali; na
7. Wawakilishi wa Miko

Sifa zinazotakiwa ili kuweza kuteuliwa kugombea ni kuwa mwanachama hai uliyesajiliwa katika Daftari la Mawakili wa Serikali na kulipa Ada ya Uanachama kwa mwaka husika wa uchaguzi pamoja na sifa nyingine zilizoanishwa katika Kanuni za Usimamizi na Uendeshaji wa Chama cha Mawakili wa Serikali T.S. Na. 529 la Mwaka 2019.

Wanachama wenye sifa wanashauriwa kuomba nafasi hizo kwa kujaza fomu na kuziwasilisha kwa Katibu wa Kamati ya Uchaguzi zikiwa zimesainiwa ipasavyo na Mgombea pamoja na Wadhamini. Fomu hizo zinapatikana katika tovuti ya Chama na Tovuti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa vikoa vya www.tpba.go.tz na www.oag-mis.go.tz. Fomu zilizojazwa kikamilifu zitumwe kwa Wakili Ludovick Ringia kupitia l.ringia@bunge.go.tz na nakala kwa Wakili Rashid Said kupitia rashid.said@osg.go.tz

Mwisho ya kurudisha fomu ni siku ya Ijumaa tarehe 5 Juni, 2026 saa 5.59 usiku na Uchaguzi utafanyika siku ya Ijumaa tarehe 26 Juni, 2026 katika Ukumbi wa AICC mkoani Arusha.

Kwa maswali na ufafanuzi wasiliana na Kamati ya Uchaguzi kupitia barua pepe l.ringia@bunge.go.tz, rashid.said@osg.go.tz au simu namba 0714560460 au 0628928553.

Hilda N. Kabissa

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi

15 Mei, 2026